HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI WA KUAHIRISHA MKUTANO WA TANO WA BUNGE LA 13 BUNGENI, DODOMA TAREHE 06 NOVEMBA, 2026

1.0 UTANGULIZI NA PONGEZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia hatua hii ya kuhitimisha shughuli zetu za Bunge. Ninapenda kutoa shukrani na pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa umahiri, maono na uzalendo mkubwa.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya uongozi wake, Serikali imeendelea kutekeleza kwa mafanikio makubwa ajenda ya maendeleo ya Taifa kupitia uimarishaji wa uchumi, utoaji wa huduma za kijamii na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Niwapongeze pia viongozi wengine wakuu, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kazi nzuri wanazozifanya.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, napenda kukupongeza wewe binafsi, pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika

na Wenyeviti wa Bunge, kwa kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa.

2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA MKUTANO WA BUNGE

4. ***Mheshimiwa Spika,*** leo, tunapohitimisha shughuli za Mkutano wa Tano wa Bunge la 13, tumefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali, ikiwemo wajibu wa msingi wa kujibu maswali na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge. Vilevile, Bunge limejadili na kupitisha taarifa za Kamati ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, pamoja na miswada ya sheria na maazimio mbalimbali kama yalivyoainishwa katika hotuba yangu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako Tukufu limepokea na kujadili taarifa za Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2024/2025. Vilevile, limepokea taarifa ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu uwekezaji na mitaji ya umma kwa mwaka 2024/2025.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Nalipongeza Bunge lako Tukufu kwa kuchambua kwa kina hoja zote za ukaguzi zilizohusu matumizi ya

fedha za umma, pamoja na kutoa maazimio ambayo kimsingi ni maelekezo mahususi kwa Serikali.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa salamu za pole kwa wananchi wote walioathiriwa na majanga mbalimbali ikiwemo ajali na majanga mengine yaliyosababisha upotevu wa maisha, majeruhi na uharibifu wa mali. Nisisitize umuhimu wa kuendelea kuimarisha mifumo ya kujiandaa, tahadhari, uokozi na utoaji wa misaada kwa waathirika wa maafa.

3.0 SHUGHULI ZA BUNGE

8. ***Mheshimiwa Spika,*** leo tunapohitimisha shughuli za Mkutano wa Tano wa Bunge la 13, tumefanikiwa kutekeleza masuala mbalimbali, ikiwemo wajibu wa msingi wa kujibu maswali na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge. Vilevile, Bunge limejadili na kupitisha Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, pamoja na miswada ya sheria ya serikali na maazimio mbalimbali.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** mkutano huu, ulijadili na kupitisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2027/2028 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028. Kwa upande wa maswali na majibu Wabunge waliuliza na kujibiwa maswali ya msingi **127**, maswali ya

nyongeza **414**, pamoja na maswali **6** ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

Miswada

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Miswada, Bunge lako Tukufu limepokea na kujadili miswada sita ambayo iliyosomwa kwa mara ya kwanza kama ifuatavyo:

Moja: Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3), Bill 2026]*;

Mbili: Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4), Bill 2026]*;

Tatu: Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Madini wa mwaka 2026 *[The Mining (Amendment) Bill, 2026]*;

Nne: Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2026 [The Environmental Management (Amendment) Bill, 2026];

Tano: Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Sekta ya Famasi wa mwaka 2026 *[The Pharmacy Sector Laws (Amendment) Bill, 2026]*; na

Sita: Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Usafiri Majini Tanzania wa mwaka 2026.

Azimio la Bunge

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Kanuni ya 64 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, Bunge lilipokea na kupitisha maazimio matatu kama ifuatavyo:

Moja: Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Kuridhia na Kuwezesha kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika Jijini Arusha kuanzia Tarehe 5 hadi 9 Oktoba 2026. Ambalo liliwasilishwa tarehe 27 Oktoba, 2026 na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Jimbo la Mtama;

Mbili: Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa wa Sukari wa Mwaka 1992 (International Sugar Agreement of 1992); na

Tatu: Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Tanzania Kujiunga na Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama wa Anga mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2014 (Mkataba wa Malabo).

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako tukufu limepokea na kujadili Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kuhusu hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa

Fedha 2024/2025. Vilevile, lilipokea Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji na Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** ninalipongeza Bunge lako tukufu kwa kuchambua kwa kina hoja zote za ukaguzi zinazohusu matumizi ya fedha za umma. Pamoja na kutoa maazimio ambayo kimsingi ni maelekezo mahsusi kwa Serikali.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ripoti ya CAG, ninatambua hisia za waheshimiwa wabunge na wananchi kuhusu taarifa ya ubadhirifu wa fedha za serikali. Waheshimiwa wabunge wamechangia kwa hisia kubwa na kuonesha jinsi gani wana uchungu na rasilimali za Taifa letu.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** serikali imeendelea kufanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Vilevile, serikali itaendelea kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na Bunge lako tukufu kupitia maazimio na hoja zilizowasilishwa.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kulihakikishia bunge lako tukufu kuwa serikali itafanyia kazi matokeo ya taarifa za Ukaguzi na watakaothibitika kufanya ubadhirifu watachukuliwa hatua kali za kinidhamu, za kiutumishi na kisheria kwa mujibu wa sheria. Niwakumbushe watumishi wote kuwa, fedha za umma ni

kodi za wananchi hivyo serikali haitawafumbia macho wale watakaobainika kufanya ubadhirifu.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawakumbusha Maafisa Masuuli na Watendaji wote wa Serikali kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma kwa mujibu wa mpango na bajeti. Lengo likiwa ni kutokusababisha uwepo wa hoja za ukaguzi zinazoweza kuepukwa wakati wa ukaguzi.

4.0 USIMAMIZI WA FEDHA NA RASILIMALI ZA UMMA

18. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ninatambua hisia za Waheshimiwa Wabunge na wananchi kuhusu taarifa za matumizi ya fedha za Serikali. Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa hisia kubwa na kuonesha namna walivyo na uchungu na rasilimali za Taifa letu. Wabunge katika Bunge lako Tukufu wanawawakilisha vyema wananchi wa Tanzania, hususan katika usimamizi wa rasilimali na kuisimamia Serikali.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kufanyia kazi mapendekezo yote yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuanzia kujibu hoja za ukaguzi hadi kuchukua hatua kwa hoja zitakazokosa majibu ya kuridhisha. Serikali itazingatia mapendekezo yote yaliyotolewa na Bunge lako Tukufu kupitia maazimio na hoja zilizowasilishwa.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba Serikali itafanyia kazi matokeo ya taarifa za ukaguzi. Watakaobainika kufanya ubadhirifu watachukuliwa hatua kali, kama ambavyo Mheshimiwa Rais amekwisha kuelekeza kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutopepesa macho anapofanya ukaguzi. Niwakumbushe watumishi wote kuwa fedha za umma ni kodi za wananchi. Serikali haitafumbia macho wale watakaobainika kufanya ubadhirifu.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** niwakumbushe Maafisa Masuuli na watendaji wote wa Serikali kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma kwa mujibu wa mipango na bajeti, ili kuepusha hoja za ukaguzi na upotevu wa fedha za umma.

5.0 MIKUTANO YA KIMATAIFA NA UTALII WA MIKUTANO

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha hivi karibuni, nchi yetu imebahatika kuwa mwenyeji wa wageni wengi na mikutano mikubwa ya kimataifa. Kwa namna moja au nyingine, hali hiyo imeendelea kuimarisha utalii wa mikutano na kukuza uchumi. Kwa mara nyingine, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia na kuwezesha kufanyika kwa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani, IPU, jijini Arusha. Kama

unavyofahamu, mkutano huo umevutia uwekezaji na kutangaza diplomasia ya nchi yetu.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Nitumie Bunge lako Tukufu kumpongeza sana Rais wa IPU aliyemaliza muda wake, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi chake cha uongozi wa miaka mitatu. Nakupongeza pia wewe, Mheshimiwa Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa shughuli za Mkutano wa 153 uliofanyika Arusha.

6.0 UZINDUZI WA MJI WA SERIKALI NA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI DODOMA

24. ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 30 Oktoba, 2026, itabaki kuwa siku ya kihistoria kwa Taifa letu, ambapo Mheshimiwa Rais alizindua Mji wa Serikali uliopo Mtumba, jijini Dodoma. Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua hiyo kubwa na kutoa maelekezo yafuatayo:

Moja: Wizara na taasisi zote zitekeleze maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa siku ya uzinduzi wa Mji wa Serikali.

Mbili: Shughuli zote zifanyike katika majengo ya Mji wa Serikali. Tuache kuendelea kutumia majengo ya kukodi kwa kuwa majengo ya Serikali yamekamilika.

Tatu: Shughuli za Serikali zifanyike Dodoma, Makao Makuu ya nchi yetu. Kwa kuwa ofisi zimekamilika, tuache kuendesha ofisi sambamba za Dodoma na Dar es Salaam. Makao Makuu ya nchi yetu ni Dodoma.

Nne: Halmashauri ya Jiji la Dodoma, kwa kushirikiana na wadau wa usafirishaji, ihakikishe usafiri wa umma unapatikana kwenda Mji wa Serikali ili kuwawezesha wananchi kufika kupata huduma.

7.0 MSHIKAMANO WA KITAIFA NA MCHAKATO WA MABADILIKO YA KATIBA

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mjadala wa Bunge lako Tukufu, zilijitokeza hoja kuhusu mabadiliko ya Katiba. Katika kufikia azma ya kuwa na mstakabali wa kitaifa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameendelea kukutana na makundi mbalimbali ya kijamii, yakiwemo viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini, wazee na wadau wengine wa kitaifa.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** mazungumzo hayo yanahusu mshikamano, maridhiano, kuimarisha amani na umoja wa Watanzania. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa nia hiyo njema kwa nchi yetu. Pamoja na suala la mshikamano na

maridhiano, Serikali imeendelea na maandalizi ya mchakato wa mabadiliko ya Katiba, ambao utakuwa shirikishi kama ambavyo Mheshimiwa Rais alisema wakati akizindua Bunge lako Tukufu.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeshatoa tamko mara kadhaa kuhusu mchakato huo, ambao inaupa uzito mkubwa na umuhimu wa kipekee, ikizingatiwa kuwa ni ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais na iliyowekwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025. Mtakumbuka kuwa Mheshimiwa Rais alitoa mwongozo wa namna ya kuliendea jambo hili.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwahakikishia Watanzania wote kuwa suala la marekebisho ya Katiba ni jambo la msingi na Serikali chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan inalipa uzito, kama alivyoahidi wakati akizindua Bunge. Maelekezo yote aliyoyatoa, pamoja na mapendekezo mbalimbali yaliyowasilishwa, yatazingatiwa. Ndiyo maana Serikali inasisitiza taratibu zote zifuatwe ili tupate marekebisho yatakayokuwa na maana kubwa kwa Taifa.

8.0 TAHADHARI KUHUSU HALI YA EL NIÑO

29. ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 28 Aprili, 2026, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ilitoa taarifa kuhusu mwenendo wa hali ya El Niño. Kwa mujibu wa uchambuzi wa kisayansi uliotolewa na

Mamlaka hiyo, kuna uwezekano mkubwa wa hali ya El Niño kuendelea.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa hizo zinaeleza kuwa ongezeko la joto la bahari la nyuzi joto 0.5 juu ya wastani ni ishara ya uwepo wa El Niño. Ongezeko la joto lililoendelea kuripotiwa hadi tarehe 1 Novemba, 2026, linaonesha uwepo wa hali hiyo na uwezekano wa madhara yanayoweza kujitokeza.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na utabiri huo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kujiandaa. Niendelee kutoa rai kwa wananchi kuzingatia tahadhari zinazotolewa ili kuepusha majanga makubwa yanayoweza kujitokeza. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa wananchi ambao tayari wamepata madhara yanayotokana na hali hiyo katika baadhi ya mikoa ambako taarifa za matatizo zimepokelewa.

9.0 UJENZI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU YA BARABARA

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mjadala wa Bunge lako tukufu, zilijitokeza pia hoja kuhusu miundombinu, hususan barabara. Bunge lilipitisha na kuridhia fedha zielekezwe moja kwa moja katika Mfuko wa Barabara ili kuwezesha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara pamoja na malipo ya wakandarasi.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** uamuzi huo umeongeza kasi na uhakika wa utekelezaji wa miradi ya barabara, pamoja na malipo ya madeni ya wakandarasi. Hatua hiyo imewezesha pia miradi kuanza kutekelezwa kwa uhakika. Serikali itaendelea kufanya matengenezo na maboresho ya barabara, ikizingatia barabara kuu za kiuchumi na maeneo mahususi yanayochochea uchumi nchini. Hatua hii inazingatia ujenzi kwa awamu na kutoa kipaumbele kwa barabara zilizoharibika.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** nilihakikishie Bunge lako tukufu na Waheshimiwa Wabunge kuwa, kwa barabara ambazo mmezizungumzia sana kutokana na uharibifu, tayari wakandarasi wamepatikana. Hatua inayofuata ni utekelezaji wa ukarabati ili zisiathiri mtiririko wa shughuli za kiuchumi nchini.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara hizo ni pamoja na Babati–Singida, Igawa–Tunduma, Mwanza–Sirari, Dar es Salaam–Kilwa–Lindi–Mtwara na Dodoma–Iringa, pamoja na barabara nyingine kuu. Tayari wakandarasi wamepatikana na wako katika hatua ya kupeleka mitambo ili kuanza kazi.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe maelekezo kwa mamlaka zinazosimamia miundombinu ya barabara nchini kuainisha maeneo yenye uharibifu na kuendelea kuyaboresha. Maboresho hayo yazingatie uharibifu uliopo pamoja na tahadhari za mvua.

Kazi hiyo iende sambamba na matengenezo ya barabara za wilaya na vijijini zinazosimamiwa na TARURA.

10.0 ULINZI WA MAENEO YA HIFADHI NA UTATUZI WA MIGOGORO

37. M*heshimiwa Spika,* amani na mshikamano vimeendelea kuwa tunu ya Taifa letu. Ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na urithi tulioachiwa na waasisi wa Taifa letu. Tunu hiyo imeendelea kulindwa chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninatoa pongezi kwa jitihada zake alizozifanya hadi sasa.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, kumekuwa na migogoro katika maeneo mbalimbali, ikihusisha maeneo yaliyohifadhiwa, wakulima na wafugaji, pamoja na wafanyabiashara wadogo. Nitumie fursa hii kuzungumzia kwa uchache masuala hayo.

10.1 Maeneo yaliyohifadhiwa

39. ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwa na matukio ya wananchi kuingiza mifugo katika maeneo yaliyohifadhiwa na kusababisha uharibifu katika shoroba za wanyamapori. Hali hiyo imechangia pia matukio ya wanyamapori kuvamia makazi na mashamba ya wananchi na kuhatarisha maisha ya binadamu. Katika baadhi ya

maeneo, uvamizi wa hifadhi umeambatana na kuwadhuru askari wa uhifadhi na wa misitu.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe wito kwa wananchi kutoingia kinyume cha sheria katika maeneo yaliyohifadhiwa na kuheshimu alama na mipaka iliyowekwa ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima. Kadhalika, nazielekeza mamlaka za uhifadhi kuendelea kushirikiana na wananchi kulinda maeneo yaliyohifadhiwa na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara. Mamlaka hizo ziepuke kutumia nguvu kupita kiasi katika kushughulikia matukio yanayoweza kuhatarisha maisha ya binadamu.

10.2 Migogoro ya wakulima na wafugaji

41. ***Mheshimiwa Spika,*** tumeendelea kushuhudia migogoro baina ya wakulima na wafugaji inayochochewa na uvamizi wa maeneo yasiyostahili. Tunakumbuka tukio lililotokea mkoani Ruvuma, lililosababisha baadhi ya wananchi kupoteza maisha na wengine kujeruhiwa.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kutoa pole kwa wananchi na familia zilizopata madhara hayo. Hata hivyo, nitoe maelekezo kwamba Serikali haikubaliani na tabia ya baadhi ya wananchi kujichukulia sheria mkononi. Kwa jambo lolote linalojitokeza, tusijichukulie sheria mkononi. Kufanya hivyo ni kinyume cha sheria na kunaweza kusababisha visasi na mapigano ndani ya jamii.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawaelekeza pia wafugaji waishi na wakulima kwa kufuata taratibu zilizowekwa katika shughuli zao za kila siku. Wafugaji wasilishe mifugo kwa makusudi katika mashamba ya wakulima, kwa kuwa kufanya hivyo ni kukiuka sheria na kuchochea migogoro.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** niwakumbushe wananchi wote kuwa kosa la mfugaji mmoja lisichukuliwe kuwa kosa la wafugaji wote. Kadhalika, kosa la mkulima mmoja lisichukuliwe kuwa kosa la wakulima wote. Kufanya hivyo kunachochea uhasama kati ya jamii hizi mbili, ambazo zote ni jamii za Watanzania. Vilevile, nawaelekeza viongozi wa serikali za mitaa, vijiji, kata na wilaya kusimamia vema matumizi bora ya ardhi ili kuepusha migogoro inayoweza kuzuilika.

11.0 PONGEZI KATIKA SANAA NA MICHEZO

45. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa sanaa na michezo, niungane na Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza Watanzania mbalimbali na timu zetu za Taifa zilizofanya vizuri. Ninawapongeza washiriki wetu waliopata mafanikio katika mashindano ya *Miss Grand International* na *Miss International*.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio hayo, pamoja na ushindi wa timu zetu katika mashindano mbalimbali, yameleta manufaa

makubwa kwa nchi yetu. Niendelee pia kuzipongeza timu nyingine zote zilizopata ushindi katika mashindano yaliyoshiriki.

12.0 MAELEKEZO MAHUSUSI

47. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijamaliza, nitoe maelekezo mahususi yafuatayo:

Moja: Utekelezaji wa maazimio ya Bunge

Ninaziagiza wizara zote kuandaa kwa wakati taarifa za utekelezaji wa maazimio yote yaliyotolewa na Bunge na kuziwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, ili ziweze kuunganishwa na kuwasilishwa kama taarifa ya Serikali Bungeni. Maelekezo na maazimio ya Bunge yanapaswa kufanyiwa kazi.

Mbili: Ushauri wa kitaalamu kwa wakulima

Nitoe rai kwa wananchi, hususan wakulima, kuendelea kufuatilia ushauri wa kitaalamu kuhusu mazao yanayofaa katika mazingira ya mvua nyingi na kutumia fursa zitakazojitokeza.

Tatu: Upatikanaji wa pembejeo

Wizara ya Kilimo iendelee kuimarisha usimamizi wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo ili ziweze kuwafikia wakulima kwa wakati.

Nne: Usimamizi wa sekta ya fedha

Ninaielekeza Benki Kuu ya Tanzania kuendelea kusimamia sera ya fedha na kutekeleza jukumu lake la kuratibu sekta ya huduma za fedha. Nitoe msisitizo kwa wananchi na wafanyabiashara kuendelea kupata uelewa wa masharti na vigezo vya huduma za fedha, ili waepuke kuingia katika mikataba yenye masharti yanayoweza kuwaumiza.

Tano: Utatuzi wa changamoto za wananchi

Ninaielekeza TAMISEMI na mamlaka za serikali za mitaa kuendelea kuimarisha utaratibu wa kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

13.0 MAFANIKIO YA VILABU VYA SOKA

48. ***Mheshimiwa Spika,*** nimalizie kipengele cha sanaa na michezo. Kama unavyokumbuka, nchi yetu imefanikiwa kupeleka vilabu vinne vya soka la wanaume katika hatua ya makundi ya mashindano ya Afrika.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** Ni jambo la kujivunia, kwa kuwa kwa miaka miwili mfululizo Tanzania imekuwa na vilabu vinne katika hatua ya makundi. Simba na Yanga zimefuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Kwa upande mwingine, Azam na Singida BS zimefuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho

Afrika. Nitumie fursa hii kuvipongeza na kuvitakia kila la heri katika hatua inayofuata.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, nivipongeze vilabu vyote vinavyoshiriki Ligi Kuu ya Tanzania. Kipekee, niipongeze timu ya Simba ambayo, baada ya kukosa ushindi kwa muda mrefu, hatimaye ilipata ushindi wa mabao mawili kwa moja katika mchezo wa Ligi Kuu uliofanyika tarehe 10 Oktoba, 2026. Niwaambie washindani wao Yanga kwamba asiyekubali kushindwa si mshindani. Nawapongeza sana kwa kuwa wameutawala mchezo huo kwa muda mrefu.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** ni ukweli usiopingika kwamba, baada ya kukosa ushindi kwa mara sita mfululizo, Simba wameonesha uvumilivu mkubwa. Uvumilivu huo umezaa matunda baada ya kupata ushindi katika mchezo nilioutaja. Niwatakie kila la heri Wanasimba, na watambue kwamba kuimba ni kupokezana.

14.0 HITIMISHO NA HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

52. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu, niwatakie Waheshimiwa Wabunge kila la heri watakaporejea majimboni kwao. Nendeni mkaeleze shughuli zilizofanyika, yakiwemo maazimio na miswada tuliyoipitisha, pamoja na manufaa ambayo wananchi watapata kutokana na maazimio na sheria hizo.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 26 Januari, 2027, saa tatu kamili asubuhi, katika ukumbi huu, hapa jijini Dodoma.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.